

**MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KILICHOKETI TAREHE
25/11/2021 KATIKA UKUMBI MDOGO WA HALMASHAURI**

WAJUMBE WALIOHUDHURIA

- | | |
|-------------------------|------------|
| 1. FRANCIS MAGHEMBE | MWENYEKITI |
| 2. HONEST WILLIAM | KATIBU |
| 3. DR. MHAGAMA INNOCENT | MJUMBE |
| 4. RAJAB BOGWA | MJUMBE |
| 5. APOLINARY SEIYA | MJUMBE |
| 6. VOSTER MGINA | MJUMBE |

WAALIKWA

- | | |
|-------------------|----------------|
| 1. TINGA A. TINGA | KAIMU MHANDISI |
| 2. GASPAR KALINGA | MWANASHERIA |

AGENDA ZILIZOJADILIWA

1. KUFUNGUA KIKAO
2. KUTHIBITISHA AGENDA
3. KUPITISHA NJIA YA UNUNUZI YA UJENZI WA MADARASA 16 YA SHULE ZA SEKONDARI NA UJENZI WA BWENI LA WANAFUNZI WENYE MAHITAJI MAALUMU KATIKA SHULE YA MSINGI YA AMANI.
4. KUFUNGA KIKAO

AGENDA NA. 1: KUFUNGUA KIKAO

Mwenyekiti alifungua kikao saa 4:00 asubuhi kwa kuwakaribisha wajumbe wote nakutaka kuchangia mada zitakaziwasilishwa kwa ajili ya kuyatolea maamuzi ambayo yatasaidia katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Halmashauri.

AGENDA NA 2; KUTHIBITISHA AGENDA

Wajumbe waliridhia agenda hizoziweze kujadiliwa.

AGENDA NA. 3: KUPITISHA NJIA YA UNUNUZI YA UJENZI WA MADARASA 16 YA SHULE ZA SEKONDARI NA UJENZI WA BWENI LA WANAFUNZI WENYE MAHITAJI MAALUMU KATIKA SHULE YA MSINGI YA AMANI.

Katibu aliwaeleza wajumbe kuwa Halmashauri imepokea fedha kiasi cha shilingi 400,000,000/= ikiwa ni fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kama ilivyoainishwa hapo chini:-

- Ujenzi wa vyumba vya madarasa 16 – 320,000,000/=
- Ujenzi wa Bweni la wanafunzi wenye mahitaji maalumu – 80,000,000/=

Katibu aliwaelekeza wajumbe kwamba kutokana na kazi hizi kutofanyika eneo moja na kwa kuzingatia Sheria ya manunuzi ya mwaka 2011 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2016 kifungu namba 64 (5), Kitengo cha manunuzi kinapendekeza kazi hii ifanyike kwa mfumo wa Force Account. Pia katika utekelezaji huo shule zilizopatiwa fedha hizo zinatakiwa kufuata Muongozo uliotolewa na PPRA, muongozo Na.PPRA:GL/05/2020/FA wa tarehe 22/05/2020

Maamuzi ya Bodi ya Zabuni

Bodi ya zabuni iliridhia matumizi ya mfumo wa Force Account katika utekelezaji wa miradi tajwa hapo juu, na kusisitiza wajumbe wote wakamati watakochaguliwa kutekeleza miradi tajwa hapo juu wajengewe uwezo.

AGENDA NA 4 : KUFUNGA KIKAO

Mwenyekiti alifunga kikao saa 5.35 na kuwashukuru wajumbe kwa michango yao pamoja na maoni waliyotoa kwa ajenda iliyowasilishwa.

UMETHIBITISHWA

Saini
Mwenyekiti

Saini
Katibu

Tarehe.....6/12/2021.....